



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KDC/L.20/22/17

24 Mei, 2022.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza **nafasi 4** kwa kada inayoonekana hapa chini:-

1.KATIBU MAHUSUSI III (NAFASI 04) TGS B SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha IV au VI
- Awe na cheti cha Astashahada (**Technician Certificate – NTA Level 5**) cha Secretarial Studies kutoka katika chuo cha Utumishi wa Umma chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E mail na Publisher.
- Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili.
- Awe amefaulu somo la Hati Mkato la Kiingereza na Kiswahili maneno 80 kwa dakika moja.

KAZI NA MAJUKUMU

- vii.) Kuchapa barua na nyaraka mbalimbali.
- viii.) Kusaidia kutunza kumbukumbu za matukio, miadi, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanya kazi na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- ix.) Kusaidia kuwapokea wageni na kuwasikiliza shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- x.) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika kazi.
- xi.) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu husika.
- xii.) Kutekeleza kazi zote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

MASHARTI YA JUMLA

- i.) Awe na umri wa miaka 18 au zaidi na asiwe na umri unaozidi miaka 45.
- ii.) Awe na afya njema, mchapakazi na mwenye utayari wa kufanya kazi mahali popote Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.
- iii.) Unatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia kutoka Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa NIDA
- iv.) Mwombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni (Passport size) iliyoandikwa jina kwa nyuma.
- v.) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi yanayojoitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- vi.) Waombaji wote waambatanishe nakala ya vyeti halisi vya kidato cha IV na VI kwa wale walifika kiwango hicho, masomo na Taaluma (**Technician Certificate – NTA Level 5**), Transcript ya cheti cha taaluma na cheti cha kuzaliwa. Mwombaji atakayewasilisha "Result Slip", "Statement of Result", "Provisional Result", au "Transcript" bila nakala halisi ya cheti cha Taaluma maombi yake hayatakubaliwa.
- vii.) Kwa waliosoma nje ya Nchi Elimu ya Kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).
- viii.) Maombi yasiyosingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa.
- ix.) Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali **TGS "B"**.
- x.) Maombi yaandikwe kwa mkono na yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani iliyotajwa hapo chini.
- xi.) Mwombaji awe ambaye hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- xii.) Maombi yote yatumwe kuanzia tarehe ya tangazo hili Tarehe **24/5/2022** hadi **06/06/2022** Aidha maombi yote hayatapokelewa Mkononi.

MUHIMU: KUMBUKA KUAMBATANISHA BARUA YAKO YA MAOMBI YA KAZI ILIYOAINISHWA PAMOJA NA VYETI VYA ELILMU (TECHNICIAN CERTIFICATE – NTA LEVEL 5).

MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa,
S.L.P 65,
KILOSA



Kisena M. Mabuba

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

KILOSA
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KILOSA

Nakala: Mbao za matangzo,